

Msumbiji yazidi kufye ka magaidi

Uhuru 25/2/88

U. 25/2/88

MAPUTO, Msumbiji

MAJESHI ya serikali ya Msumbiji
waliwaua magaidi 37 na kuharibu kambi

zao kadhaa katika jimbo la Inhambane
lililoko kusini mwa nchi hiyo mwezi
aliopita, Shirika la habari la Msumbiji
(AIM) liliripoti jana.

Lilisema magaidi 17 wa MNR
waliwaua katika wilaya ya Homoine
ambako magaidi waliwaua zaidi ya raia
400 na wengine 40 katika wilaya ya
Morrumbene.

Shirika hilo likikariri habari za kijeshi
lilisema kambi moja ya magaidi hao il-
ikamatwa na majeshi ya serikali huko
Guele, katika wilaya ya Panda.

Mjini Nairobi, Kenya, Shirika la
Mpango wa Chakula la Umoja wa

Mataifa (WFP) limesema linatarajia
kuona wakimbizi wengi kutoka Msum-
biji kwenda nchi jirani yake mwaka huu
kutokana na uhaba wa chakula na
ukatili unaendeshwa na magaidi hao.

Taarifa iliyopokewa Nairobi kutoka
Rome, Italia, makao makuu ya shirika
hilo, ilisema idadi ya caa wa Msumbiji
katika Malawi itaongezeka na kuikia
600,000 ifikapo Desemba kutoka idadi
ya 420,000 waliopo sasa.

Huko Swaziland kuna wakimbizi
22,500 wa Msumbiji, Zambia 30,000,
Zimbabwe 64,500 na Tanzania 72,000,
taarifa hiyo ilisema.